**PEACE BRIGADES INTERNATIONAL**
International Office
Development House, 56-64 Leonard Street
Tel: 44 (0)20 7065 0775 London EC2A 4LT
Email: admin@peacebrigades.org
Website: www.peacebrigades.org

# UKADIRIZI WA UWEZEKANO NA UMANUFAA WA MPANGO WA UANDAMANAJI WA KULINDA WAPIGANIA HAKI ZA BINADAMU NCHINI KENYA

## UKADIRIZI WA UWEZEKANO NA UMANUFAA WA MPANGO WA UANDAMANAJI WA KULINDA WAPIGANIA HAKI ZA BINADAMU NCHINI KENYA

## MUHTASARI

**Peace Brigades International**

**Julai 2012**

**Translated by:**
Lena Muyanga
Advocate of the High Court of Kenya

**KUHUSU PBI**

Tangu mwaka wa 1981, PBI imeunga mkono jamii tofauti na maelfu ya watu katika nchi kumi na moja za Amerika Kusini na zinginezo katika bara la Asia. Tunalinda wapigania haki za kibinadamu wanaotetea walio nyimwa haki zao za kimsingi, walio fukuzwa makwao na pia wale waliotishwa. Tunafanya kazi kwa ombi la hawa wapigania haki na kulingana na mahitaji yao. Uandamanaji ili kulinda ndiyo mbinu kuu ya shirika letu- mbinu hii hushirikisha umahiri maalum maarifa ya kijamii na kushurutisha mataifa ya kijamii. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba wapigania haki za kibnadamu wanaweza kufanya kazi yao bila hofu na pia waweze kuchangia kwa haki ya jamii na amani na usalama.

**HISTORIA**

Kwa sasa, PBI haija tekeleza mradi wowote barani Afrika ingawa tumepata maombi ya usaidizi kutoka wanaopigania haki za kibinadamu kutoka pande tofauti barani Afrika. Jambo hili lilituongoza kukadiria uwezo wa PBI kuanzilisha mradi nchini Chad hapo mwaka wa 1993 ingawa juhudi zetu hazikufua dafu. Katika mwaka wa 2009-10, tuliendeza utafiti wa mahitaji ya ulinzi ya wanaopigania haki za kibinadamu barani Afrika. Utafiti huu ulifanywa nchini Kenya mwaka wa 2009 na ulipendekeza kwamba, mbinu za PBI za utekelezaji wa kazi wa uandamanaji ili kulinda ulikuwa na uwezo wa kuridhisha mahitaji ya ulinzi nchini Kenya.

**MUHTASARI**

Katika mwaka wa 2011, PBI ilianzisha Kamati ya Kenya Project Exploratory Committee (KPEC), iliyohusisha wapigania haki za kibinadamu wa PBI na wataalamu wa humu nchini Kenya ili waweze kutafakari kwa kina matokeo ya utafiti uliokuwa umetekelezwa katika mwaka wa 2009.

Utafiti huu ulibainisha ya kwamba; kulikuwa na haja ya mpango wa uandamanaji, kwa sababu watetezi wa haki za kibinadamu wanakabiliwa na changa moto za kunyanyaswa. Mbinu hizi za PBI zina manufaa kwa mfano na ni kwa sababu hii watetezi wa haki na washika dau wa mataifa ya kigeni wanaweza kukaribisha uamzi wa kuanzisha shirika la kulinda watetea haki za kibinadamu nchini Kenya. Kwa sababu hii mashirika yote ambayo yanafanya kazi nchini yatapaswa kuelewa jinsi ya keundeleza operesheni zao katika sehemu ambazo kuna makundi haramu ya kivita. Utafiti wa 2011, uliendelezwa kukadiria mahitaji ya ulinzi ya watetea haki za kibinadumu na uwezekano na matokeo ya andamanaji uhifadhi wa PBI nchini Kenya.

Kamati la KPEC, liliendeleza utafiti na likasafiri hadi maeneo tofauti ya nchi kati ya miezi ya Septemba na Oktoba 2011. KPEC Ilitumia vipimi na maswali nyeti

kujulisha ukadirizi ili kudhihirisha kama PBI ingeanzisha mradi Kenya na matokeo haya yameangaziwa kwa kina katika ripoti kuu.

Utafiti ulitambua mahitaji ya watetea haki na ikapata ya kwamba hali inayofaa ya uandamanaji wa kulinda ilikuwa inapatikana maeneo tofauti ya Kenya katika mikoa ya Nairobi, magharibi mwa Kenya na Mombasa. Ilionyesha ya kwamba kulikuwa na uwezo wa kazi ya PBI kufua dafu. Matokeo makuu ya utafiti huu yalikuwa:

**HALI YA WATETEA HAKI ZA KIBINADAMU NCHINI KENYA**

Ingawaje hali nchini Kenya imeimarika tangu utafifiti wa mwisho wa PBI mnamo mwaka wa 2009, ambayo iliangazia msimu wa vita iliyozuka baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007, watetea haki za kibinadamu wanawndelea kukabiliwa na changa moto na hali ya hatari ambayo inazuia kazi yao.

Hali ya kutoheshimu haki za kibinadamu imekidhiri mno (ikiwapo kutoheshimu watetea haki), vitisho na kuhamishwa kwa lazima pia si mambo mapya. Visa vya kuchunguzwa na serikali na watu kibinafsi pia vimeripotiwa na ofisi zimevamiwa na kompyuta kuvunjwa kwa nia ya kutafuta taarifa na mashirika kadhaa yalishuku ya kwamba maongezi yao kwa simu yalikuwa yakisikilizwa. Kushikwa na polisi kiholela (sana sana wakati wa maandamano ya amani) ili ripotiwa mara nyingi sana katika sehemu za magharibi na Pwani mwa Kenya na watetea haki hawa hufuatwa na kutupwa korokoroni bila kupelekwa kortini na pia huitishwa hongo.

Mambo ya hatari kuu ambayo watetezi wa haki wanayo shughulikia ni kama vile vita vilivyozuka baada ya uchaguzi mkuu wa 2007, mauaji ya kiziada na polisi, vita dhidi ya ugaidi, uajibikaji, ufisadi, kuangalia kwa makini mambo ya kijamii kama vile haki za kijinsia na haki za umiliki wa ardhi.

Kazi ya wanawake ambao wanaotetea haki za kibinadamu iliangaziwa kama kuwa na changa moto tele. Ubakaji na dhulma za kijinsia ni matukio ambayo yanawakumba wanao fanya kazi katika vitongoji duni na huenezwa na watu kibinafsi. Masenge au shoga hunyanyaswa na polisi, hutupwa korokoroni mara kwa mara bila sheria kufuatwa na pia hulazimishwa kutoa pesa (mara mingi na poilisi) na hukabiliwa na ukatili.

Ilibainika wazi ya kwamba hofu ni sababu moja ambayo watetea haki za binadamu huweka sera na mikakati fulani. Mauwaji ya watetea haki wawili kutoka shirika la *Oscar Foundation* 'yaliwashtuwa' wengi katika makundi yasiyo ya kiserikali na ikawafanya baadhi ya watetezi haki za kibinadamu kuto taja majina na kufuata watu binafsi waajibike na badala yake kuanza kupigania mabadiliko ya sera ndani ya mashirika.

Kwa jumla, hakuna muungano wa watetea haki, wale wa mashinani wana hisi kutumiwa vibaya au kutozingatiwa na wale watetea haki walio ulingoni wa kimataifa. Mashirika ya kitaifa yamekosolewa kwa kutoitikia mwito wa mashirika ya mashinani, kuto yaunga mkono mashirika haya na kutofikiria mahitaji ya watetea haki wa mashinani ikizingatiwa ya kwamba ndio wako mstari wa mbele kutetea haki za kibinadamu. Jambo lingine linaloendeleza kutofautiana kati ya mashirika haya ni sababu mashirika ambayo yako Nairobi hupata 80% ya pesa za wahisani. Ukosefu wa muungano pia unashuhudiwa kati ya mashirika ya Nairobi ambayo yana wahisani na yale mashirika ya kijamii ambayo yanafanya kazi katika vitongoji duni na yale mashirika ambayo yako nje ya Nairobi. Migawanyiko hii na kutokuwa na muungano wa kitaifa wa mashirika ya kutetea haki inachangia unyonge wa watetea haki ambao wanafanya kazi mashinani na katika vitingoji duni.

**HALI YA MPANGO WA UANDAMANAJI WA KULINDA**

Serikali ina uthabiti na jinsi za uajibikaji kuitikia kilio wa ulinzi cha watetezi wa haki. Lakini serikali haijaweka mbinu zozote za kulinda watetea haki. Inaonekana ya kwamba nchi za kigeni zina nia ya kuingilia kati na kuchukua hatua ya kuwalinda watetea haki. Serikali ya Kenya inaonekana kupokea shinikizo kutoka kwa jamii ya kimataifa na viashirio vyaonyesha ya kwamba msongo kutoka humu nchini pamoja na ile ya kutoka kwa nchi za kigeni inaweza kuwa na manufaa. Hata hivyo, matukio ya hivi juzi ya watu mashuhuri kupatwa kuwa na kesi ya kujibu katika Koti ya kimataifa ya jinai, ICC, imefungua njia ambayo hisia dhidi ya mataifa ya kigeni inaenezwa. PBI inaweza kuendeleza kazi zake kutoka Kenya ingawa kunaweza kuwa na changamoto kuhusu utawala dhidi ya kuwa nchini Kenya kwa muda wa kipindi kirefu.

Hali ya usalama inaweza ruhusu PBI iwatume watu wa kujitolea katika sehemu kadhaa nchini Kenya ikiwemo Nairobi, Magharibi mwa nchi na Mombasa.(sehemu zingine kama vile mpaka wa Somalia, sehemu za juu ya Bonde la Ufa na mpaka wa Kenya na Ethiopia zinatambulika kwa kuwa hatari.)

**MAHITAJI YA WATETEA HAKI ZA KIBINADAMU NA JINSI PBI INAWEZA KUYATEKELEZA**

Mahitaji ya watetea haki za kibinadamu nchini Kenya yanajumuisha mambo kadhaa ambayo ni ya muhimu mno katika mbinu ya ulinzi ya PBI ya uandamanaji wa kuhifadhi ikiwemo; kukuza muungano wa watetea haki za kibinadamu, kuunganisha watetea haki za kibinadamu katika maeneo ya bara na pia kimataifa, kusaidia kutambuliwa kwa watetea haki halisi. Ilibainika kwamba kulikuwa na haja ya mafunzo ya ulinzi na usaidizi wa ziada. Tena, watetezi wote wa haki za kibinadamu

ambao walikutana na PBI, waliunga mkono wazo la mpango wa uandamanaji wa kulinda -wazo ambalo lilikuwa geni kwao-na wengi walitoa maoni ya dhamana jinsi ya kurekebisha wazo la uandamanaji ili itumike nchini Kenya. Wengine walifurahia hilo wazo lakini walizingatia changa moto ambazo zingekuwapo. Baadhi ya changa moto hizi ni kama vile kuthibiti hisia mbaya kuhusu watu kuandamana katika jamii fulani na zile hisia nzuri na manufaa ambayo kazi ya PBI inaweza kuleta na kuzungumuza na serikali na umoja na muungano ambao unaweza tokana na uandamanaji wa kulinda. Utafiti ulibaini ya kwamba PBI ingesaidia kujaza pengo ambalo limetambuliwa kuhusu uandamanaji wa kuhifadhi na itumie kama njia ya kuwasaidia watetezi wengine wa haki za kibinadamu katika eneo la Afrika Mashiriki kwa wakati ujao.

**MWISHO**

Kuna uwezekano wa shirika la PBI kama litakuwa limeanzisha afisi humu nchini kushiriki katika kulinda na kuunga mkono watetea haki za kibinadamu kwa muda huu ambao taharuki inatarajiwa kuwa ya hali ya juu wakati huu wa uchaguzi wa 2013. Kazi ya muda mfupi kwa msimu huo, utaisaidia PBI kufanya utafiti zaidi ili kubaini changa moto zipi zinakumba kuanzalisha mpango wa uandamanaji wa kulinda nchini Kenya na kama zinaeza shindwa. Kukaa kwa muda mrefu mashinani inaweza kusaidia kufafanua mahitaji ya watetea haki za kibinadamu wa eneo kuu la Afrika Masharikі. Ni kwa sababu hizi ripoti hii inapendekeza ya kwamba PBI ianzishe mradi wa muda mfupi nchini Kenya Katika kipindi cha 2012-2013.